035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA
# LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

   Jibu sahihi ni **D**

   **Katika karatasi ya majibu:**

   **2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

***<u>Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lililo mwafaka zaidi.</u>***

Jukumu la lugha kama wenzo wa mawasiliano _____1_____ kupuuzwa. _____2_____ kila kabila huwa na lugha yake ambayo _____3_____ kitamaduni na kimila. Ni muhimu kufahamu kuwa kiini cha lugha yoyote ile ni sauti. _____4_____ sauti hizi ni zile zinazotetemesha nyusi za koromeo yaani _____5_____. _____6_____, kuna lugha nyingi _____7_____ ulimwenguni , lengo kuu hasa huwa ni _____8_____ mawasiliano kwa namna _____9_____. Kila jamii inafaa kuithamini lugha yake bila kuionea fedheha kwani _____10_____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Haiwezi | hauwezi | haliwezi | hayawezi |
| **2.** | Angalau | lau | aghalabu | ingawa |
| **3.** | Hulitambulisha | huwatambulisha | huitambulisha | hututambulisha |
| **4.** | Mojawapo ya | baina ya | miongoni mwa | katikati ya |
| **5.** | Sighuna | mwambatano | changamano | ghuna |
| **6.** | Halikadhalika | minghairi ya hayo | ijapokuwa | waama |
| **7.** | Mote | pote | kote | kwote |
| **8.** | Kuyafaulisha | kutufaulisha | kuyatoshelezea | kututosheleza |
| **9.** | Yafaayo | ifaavyo | ifaayo | yafaavyo |

**10.** A. Mzigo u kichwani, kwapa lakutokeani jasho

B. Mwenda tezi naomo marejeo ni ngamani

C. Mwacha mila ni mtumwa

D. Mtegemea cha nduguye hufa maskini

Nilisimama tisti _____11_____ mnara wa Babeli tayari kuwaelekeza wananafunzi wenzangu. Niliviweka vitabu _____12_____ meza iliyokuwa mbele ya darasa._____13_____ kwa kuzamia msamiati wa kazi kama vile _____14_____ ambayo ni kazi mtu hujitolea kuifanya bila malipo. Aidha, niligusia kivumishi cha pekee *–enyewe* ambacho hutumika kuonyesha ubinafsi na _____15_____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | Licha ya | minghairi ya | bighairi ya | shabiku |
| **12.** | Kwenye | kwa | katika | ndani ya |
| **13.** | Nilitia fora | nilijizatiti | niling'oa nanga | nilikata kalima |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **14.** Makataa | msaragambo | ujima | kunga |
| **15.** Idadi | nafasi | kumiliki | kuashiria |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30 jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Chagua sentensi ambayo imetumia kiwakilishi cha idadi kamili.

A. Magari yale matatu yaliyohusika katika ajali yameungua.

B. Yeyote wa kwanza atakayewasili atatuzwa vyema.

C. Juma alinunua machungwa mengi akanipa mawili.

D. Wao wanavyo vyakula haba ghalani.

**17.** Chagua maelezo yaliyo sahihi.

A. Mkalimani ni anayetafsiri maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine.

B. Nyakanga ni anayewapasha tohara wavulana.

C. Mjume ni mtu stadi wa kufua visu.

D. Manamba ni wafanyikazi wa kuhama katika mashamba makubwa.

**18.** Ni orodha gani iliyo na vielezi pekee?

A. Lau, mno, bali, vile.

B. Kuliko, tena, aghalabu, kivivu.

C. Kadhaa, la kwanza, laiti, kivoloya.

D. Katu, kati ya, waama, nomi.

**19.** Chagua sentensi inayoonyesha hali ya kutendeka kwavitendo sambamba.

A. Aliniita akanipa hela nikaenda dukani.

B. Mvuvi Yule anatembea akipiga miluzi.

C. Polisi walimfumania akihesabu pesa alizoiba.

D. Ataufeli mtihani asipofanya bidii za mchwa.

**20.** Teua mapambo ya miguuni pekee.

A. Timbi, mafurungu, udodi, njuga.

B. Kidomwa, ngeu, kanta, hina.

C. Kigwe, kogo, kipini, mapete.

D. Kidani, jaribosi, hazama, wanja.

**21.** Chagua sentensi isiyo sahihi kisarufi.

A. Majanadume wale wenye miraba minne ni hodari.

B. Mwimbaji mwenye kufurahisha ni Yule.

C. Mgonjwa dhaifu ametibiwa leo.

D. Popote pale penye miti panavutia mno.

**22.** Ni chombo kipi kinaambatana na matumizi yake sahihi?

A. Jiriwa – kupima unyookaji wa ukuta.

B. Kekee – kutobolea mashimo ya mviringo kwenye mbao.

C. Maharazi – hufungwa kidoleni kwa mshonaji asidungwe na sindano.

D. Hadubini – kufanya vitu vilivyo mbali vionekane kama vilivyo karibu.

**23.** Ni upi wingi wa sentensi hii?

***Unastahili kumlipa yaya huyu wako kwa ulezi anaoufanya.***

A. Mnastahili kuwalipa mayaya hawa wako kwa malezi wanayokufanyia.

B. Mnastahili kuwalipa yaya hawa wenu kwa malezi wanayowafanyia.

C. Mnastahili kuwalipa mayaya hawa wenu kwa malezi wanayowafanyia.

D. Mnastahili kuwalipa yaya hawa wenu kwa ulezi wanaowafanyia.

**24.** Chagua sentensi iliyoakifishwa isivyofaa.

A. Nairobi – mji mkuu wa Kenya – una wakazi wengi.

B. "Musa,niazime kalamu yako," Maria akasema.

C. Shirika la msalaba mwekundu huwafaa wahasiriwa.

D. Ni nani asiyefahamu kuwa bahati ni chudi?

**25.** Chagua methali isiyolingana na maelezo haya.

***Mtu hafai kujiingiza katika mambo yasiyomhusu.***

A. Jivu usilolilalia waliwingiani paka.

B. Mzigo uko kichwani kwapa lakutokeani jasho.

C. Mla ni mla leo mla jana kalani.

D. Pilipili usiyoila yakuwashiani.

**26.** Neno **'kinachomsikitisha'** lina silabi ngapi?

A. 15

B. 8

C. 9

D. 13

**27.** Geuza kwa usemi halisi.

Mama aliniuliza mbona hatukuwa tumesafisha vyumba vyetu siku hiyo.

A. "Mbona hukusafisha chumba chako leo?" Mama akaniuliza.

B. "Mbona hamjasafisha vyumba vyenu leo?" Mama aliniuliza.

C. "Mbona hamkuwa mmesafisha vyumba vyenu leo?" Mama alituuliza.

D. "Mbona hamkusafisha vyumba vyenu leo?" Mama alituuliza.

**28.** Chagua maelezo sahihi.

A. Taya ni nyama zinazoshikilia meno kinywani.

B. Moyo husafirisha damu katika sehemu zote mwilni.

C. Kichogo ni sehemu ya juu ya kichwa.

D. Nso hutakasa damu kwa kuichuja.

**29.** Chagua sentensi iliyotumia chuku.

A. Alipasua kicheko ja radi.

B. Maimuna ni samaki kidimbwini.

C. Kiatu cha Musa kinacheka daima.

D. Nilishtuka moyo ukanisakama kooni.

**30.** Ni upi ukanusho wa:

Wanafunzi walio na bidii wanahitaji kutuzwa.

A. Wanafunzi walio na bidii hawahitaji kutuzwa.

B. Wanafunzi wasio na bidii hawahitaji kutuzwa.

C. Wanafunzi walio na bidii hawahitaji kutotuzwa.

D. Wanafunzi wasio na bidii hawahitaji kutotuzwa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Misitu ni ya aina mbili. Ipo ile ya kiasili kama Msitu wa Mau na Msitu wa Kakamega. Halikadhalika, ipo misitu ya kupandwa kama vile Kinale, Webuye na Timboroa. Misitu ni hazina kubwa kwa jamii yoyote ile. Kila mwanajamii anapaswa kujivunia misitu.

Misitu husheheni miti ya aina nyingi ambayo, pamoja na kuwa makazi ya wanyama, hutoa vyakula kama vile matunda na majani ambayo huwafaidi binadamu na viumbe wengine. Bila misitu binadamu na wanyama wangeangamia.

Isitoshe, misitu ni ivutio aula cha watalii. Watalii kutoka ndani na hata nje ya nchi huzuru misitu na mbuga mbalimbali za wanyama kujionea na kuajabia uzuri wake. Watalii hawa hulipa fedha za kigeni ambazo hutumiwa kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile kustawisha miundomsingi na miradi mingine yenye manufaa kwa taifa.

Fauka ya hayo, misitu husafisha hewa na kurembeshamandhari wanayoishi adinasi. Rangi ya kijani kibichi na maua yenye rangi tofautitofauti huyafanya mazingira kupendeza hata yakitazamiwa kwa mbali. Mandhari yasiyo na miti hayakosi urembo tu, bali huwa wazi kiasi kwamba hata mapaa ya majengo yaliyo hapo wakati mwingine hupeperushwa na upepo mkali.

Aidha, vipindi virefu vya jua huwanyima viumbe starehe na huweza kusababisha saratani ya ngozi kwa binadamu. Miti hufanya vivuli ambavyo huwakinga watu na wanyama dhidi ya miale ya jua. Isitoshe, si ajabu kuwa mahali ambapo pana miti mingi kwa kawaida hupata mvua tele hata wakati usio wa majira ya kifuku.

Sekta ya afya imefaidika si haba kutokana na miti. Matibabu ya kienyeji na hata ya

kisasa hutumia mizizi, majani na magome ya miti hutengeneza dawa. Miti kama mwarubaini hutibu ndwele nyingi. Hivi sasa magonjwa kama bolisukari, shinikizo la damu na ugonjwa wa figo **yameweza kudhibitiwa** kwa kutumia dawa zitokanazo na miti. Inasemekana kuwa hata nyoka humtibu nyoka mwenzake kwa majani.

Miti hutumiwa viwandani kutengeneza bidhaa kama vile karatasi na samani. Viwanda hivi hutoa ajira kwa maelfu ya raia, hivyo kupunguza makali ya uhaba wa nafasi za kazi nchini.

Ni wazi kuwa uhifadhi wa misitu una manufaa tumbi nzima kwa binadamu. Hata hivyo, binadamu mwenyewe ndiye anayeangamiza misitu yenyewe. Watu wenye mate ya fisi wamekata miti kiholela kwa ajili ya kupata kuni na kuchoma makaa ya kuuza. La kusikitisha ni kwamba watu hawa **hawadiriki** kupanda miti mingine kufidia ile waliyoikata. Wengine kwa kutojua wanajipalia makaa, hupanda miti ambayo inakausha vyanzo vya maji na kuchangia kuenea kwa kasi kwa jangwa. Halikadhalika, wapo warina asali ambao katika juhudi zao za kurina husababisha kuteketea kwa misitu.

Kifungu cha katiba kinachohusu mazingira na mali ya asili kinasisitiza suala la uhifadhi wa mazingira. Kila mwanajamii basi ana jukumu la kuilinda misitu na kuepuka mazoea ambayo yanaiangamiza, lau sivyo tutakuwa tunajichimbia kaburi.

31. Kulingana na ufahamu, mchango wa utalii kwa jumla ni;
    - A. Kuongeza fedha za kigeni kwenye mbuga.
    - B. Kuboresha miundomsingi kwenye misitu.
    - C. Kuimarisha uchumi wa nchi.
    - D. Kuwekeza miradi ya nchi.

32. Ni ipi hasara za kutohifadhi misitu kwa mujibu wa kifungu?
    - A. Kunyauka kwa majani, kupoteza urembo.
    - B. Kuporomoka kwa majengo, kupoteza mvuto.
    - C. Mahali pakavu, kuchukiza kwa mazingira.
    - D. Upepo mkali, kunyauka kwa maua.

33. Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?
    - A. Dawa za kienyeji huponya kabisa magonjwa mengi sugu.
    - B. Kuhifadhi misitu kunaweza kuchangia kuongezeka kwa nafasi za kazi.
    - C. Mahali penye miti mingi hupata mvua inayotegemewa kila mara.
    - D. Kuwa na vipindi vya jua kali kunaweza kusababisha saratani.

34. Kifungu kinasema kuwa miti hutumika:
    - A. Kutengenezea kawi na kuwasetiri viumbe.
    - B. Kuunda samani na kuhifadhi maji.
    - C. Kusafisha hewa na kufanikisha majengo.

D. Kuvuta mvua na kuburudisha viumbe.

35. Maana ya methali **'Mwiba wa kujichoma huambiwi pole'** imedhihirika katika kifungu kwa vile:

A. Watu ndio wanaojisababishia hali mbaya ya ukame kwa kupuuza umuhimu wa miti.

B. Watu ndio wanaojisababishia hali mbaya ya kiangazi kwakupuuza umuhimu wa misitu.

C. Watu ndio wanaojisababishia visima kwa kupanda miti isiyofaa.

D. Watu ndio wanaojichomea misitu kwa kurina asali pasipostahili.

36. Mwandishi anaonyesha kichocheo kikuu cha kukata miti ni:

A. Kuwa na haja ya kuuza makaa.

B. Kuwa na hamu ya kupata asali.

C. Kuwa na tamaa ya mali.

D. Kuwa na mahitaji ya kuni.

37. Ni jibu lipi ambalo si sahihi kulingana na **aya ya nane**?

A. Ukataji wa miti unapaswa kuandamana na mpandaji miti upya.

B. Shughuli yenye faida huweza kuishia kuwa janga.

C. Ukosefu wa maarifa unaweza kusababisha hasara.

D. Jaribio la kupanda miti linastahili kuepukwa panapotolewa maji.

38. Kulingana na **aya ya mwisho**:

A. Mazingira huhifadhiwa kupitia kwa kifungu cha katiba.

B. Mwanajamii hujiletea majuto kwa kutoepuka mienendo isiyokubalika.

C. Mazingira huharibiwa na hulka zisizofaa za binadamu.

D. Mwanajamii anastahili kufuata mshawasha wa katiba.

39. Kwa mujibu wa taarifa, 'yameweza kudhibitiwa' ina maana:

A. Yameweza kuondolewa.

B. Yameweza kuzuiliwa.

C. Yameweza kutibiwa yote.

D. Yameweza kupunguzwa yote.

40. Mada mwafaka ya kifungu hiki ni;

A. Madhara ya ukataji wa miti.

B. Jinsi ya kupanda miti.

C. Uhifadhi wa mazingira.

D. Faida za misitu.

***Soma Kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50***

Mahafali ya kufuzu kwa mke wangu yalifana sana. Baada ya kusomea shule ya msingi kwa miaka minane, ya sekondari kwa mingine minane na chuo kikuu kwa minne zaidi, **siku ya ndovu kumlamwanawe** hatimaye iliwadia. Mwamu wangu na wavyele walikuwa

na furaha isiyo na kifani kumwona kifunguamimba wao na taji la ufanisi katika taaluma ya elimu

Baada ya hafla huko chuo kikuu cha Mlima Kenya – Thika, aila, jamaa na wandani wote tulijumuika nyumbani kwao. Mlolongo wa magari ulifuatwa hadi mtaa wa Songambele. Nyamoita aliongoza njia pindi tu tulipofika akina nina kwa waume walimlaki kwa ngoma za kitamaduni nao mahirimu wakamwinua hobelahobela wakimshangilia kwa vifijo na nderemo si haba. Ndugu zake  Jitihada na Bidii wasingeweza kuficha furaha yao;walimpiga pambaja na busu huku wakitiririkwa na machozi michirizi. Nyamoita naye alionyesha **kongole** zake kwa kuchangamkia yeyote aliyekuwepo.

Tulikula maakuli yaliyoandaliwa hadi shibe yetu.'Mcheza kwao hutuzwa'chambilecho wahenga.Sote tulibaki kuachama vinywa zawadi zilipoanza kutolewa. Mwana wa watu hakupokea kitita cha ngwenje tu; tarakilishi, rukono, mavazi, vinyago na nyinginezo alituzwa. Wazee nao walimpa mawaidha huku wakimsifu kwa bidii, ari na uwajibikaji wake. Wakembe na vijulanga waiohudhuria sherehe walisihiwa wazifuate nyayo za Nyamoita, maadamu alikuwa kielelezo chema cha kuigwa. Hakika, jina jema hung'aa gizani.

"Ninayo furaha na buraha ghaya siku ya leo. Namshukuru Jalali Jalia kwa kunifikisha nilipo. Sina maneno kamili ya kuelezea hisia zangu kwa wazazi wangu. Kunizaa, kunipakata, kunikosha, kunilea na kunilipia karo hadi wa leo ni ukarimu usioelezeka. Kwa ndugu, jamaa na wasenangu nitawaombea Mola aendelee kuwanyea Baraka zake tolatola. Kwa maombi , uadilifu na kutia shime kutwa kucha. Niliamua kuacha raha ningi zizaazo karaha na kujifunga kibwebwe ili nivae gauni hili jeusi tititi. Kunao wale walioniona fala kwa kutokuwa bendera ifuatayo upepo wa shinikizo la rika. Uraibu wa vileo nikaukataa katakata na kujitwika mzigo wa nanga kwa kubukua mabuku anuwai.

Sijivishi kilemba cha ukoka wala kujishaua kuwaarifu kuwa sijatosheka na kisomo. Mwaka ujao nitarudi kuko huko chuoni kuongeza maarifa.Tayari nimepata ajira katika shule ya kibinafsi.Mwajiri wangu ameniahidi kuwa atafanya kila awezalo kufanikisha ndoto hiyo. Nitayawahi masomo hadi nikinai kiu yangu kwa kuitwa profesa kaski mosi. Nitatamatisha kwa kumshukuru kwa dhati na taadhima mpenzi wangu Kumbo aliyenitia mshawasha na makali ya kuyakumbatia masomo kama duduvule agotaye mkoche. Hati hii ya kwanza nimeipata kwa busara hii yako mpenzi. Rabana awabariki nyote.Asanteni."

41. '***Siku ya ndovu kumla mwanawe***' inamaanisha:

A. Siku ya kusafiri kwenda mjini.

B. Siku ambayo wanyama wa mwituni hukutana.

C. Siku ya kusherehekea na kufurahi.

D. Siku ambayo ndovu humwua mwanawe.

42. Kulingana na **aya ya kwanza**, aliyefuzu;

A. Ndiye mwandishi wa makala haya.

B. Alipata ufanisi katika taaluma ya elimu.

C. Alikuwa amesoma kwa miaka minane.

D. Alikuwa na mke aliyefurahi

sana.

43. Aila, jamaa na marafiki walijumuika;

A. Kabla ya sherehe ya mahafali.

B. Jijini Thika katika sherehe ya mahafali.

C. Siku mbili baada ya sherehe ya mahafali.

D. Nyumbani baada ya sherehe ya mahafali.

44. Chagua jibu ambalo si kweli kulingana na**aya ya pili**.

A. Akina mama na waume walimpiga pambaja Nyamoita.

B. Jitihada na Bidii walikuwa ndugu zake Nyamoita.

C. Waliompokea Nyamoita walifurahi sana.

D. Nyamoita alifurahia kila mmoja.

45. Maana ya kongole ni ______

A. Huzuni

B. Hisia

C. Shukrani

D. Furaha

46. Kwa mujibu wa **aya tatu**;

A. Maakuli yalikosekana katika sherehe.

B. Zawadi kochokocho zilitolewa kwa Nyamoita.

C. Vijana walimnasihi Nyamoita

D. Nyamoita alihutubia umati.

47. Ushauri uliotolewa kwa vijana ni ufuatao isipokuwa;

A. Kuoma.

B. Kuwa waadilifu.

C. Kutia shime.

D. Kufuata shinikizo la mahirimu.

48. Maana ya '***kujishaua***' ni

A. Kujipenda

B. Kuringa

C. Kujirasha maua

D. Kujipodoa

49. Kwa mujibu wa **aya ya tano**, ndoto ya Nyamoita ilikuwa;

A. Kutosheka na masomo

B. Kujivika kilemba cha ukoka na kujishaua.

C. Kupata kazi katika shule ya kibinafsi.

D. Kuendelea na msomo.

50. Kwa nini Nyamoita anamshukuru Bwana Kumbo?

A. Kwa kumpa hati ya masomo.

B. Kwa kumtia motisha ya masomo.

C. Kwa kumlipia karo ili asome.

D. Kwa kumwoa

*Kamilisha insha ya kusisimua ukianza kwa maneno yafuatayo.*

Siku ilikuchwa mbaya kwa makeke ya radi na umeme. Nami ......................................................